JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI KONDOA

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KONDOA

S. L. P 193, Kondoa-Dodoma Website; www.kondoasec.ac.tz, Email: kondoagirls@gmail.com

KUMB.NA.KGSS/FFS/VOL.1 ……. DATE: …… ……

NAMBA ZA SIMU:

1. MKUU WA SHULE: 0713-448-417
2. MAKAMU MKUU WA SHULE: 0755-983-003/0717464642

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI:……
S.L.P ……
……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KONDOA ,HALMASHAURI YA MJI KONDOA,MKOA WA DODOMA MWAKA 2018

1.0 PONGEZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka **2017** tahasusi ya…… Shule ya Sekondari ya Wasichana Kondoa ipo umbali wa Kilometa **nne(4)**, **Kaskazini- Magharibi mwa mji wa Kondoa.** Shule ipo Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma. Mji wa Kondoa upo karibu na barabara itokayo Dodoma kwenda Babati hadi Arusha.

Usafiri wa Teksi kutoka **mjini Kondoa** hadi shuleni unapatikana katika kituo cha mabasi **Kondoa,**nauli ni kati ya **shilingi 5000 na 7,000/=(**ni maelewano) kwa **"Tripu –hata muwe zaidi ya mmoja"** na sio kwa kichwa/mtu mmmoja.Pia kuna usafiri wa bajaji ambazo nauli yake ni kati ya **2000/= na 3000/=(**maelewano). Unaweza kufika shuleni hata kwa miguu ila kama utafika usiku usitembee kwa miguu.
NB: Usafiri wa boda boda haushauriwi/haufai.

Muhula wa masomo unaanza tarehe……Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe……Mwisho wa kuripoti ni tarehe…… Endapo hutaripoti hadi tarehe hiyo ya mwisho utahesabiwa kuwa umekataa nafasi uliyopewa, hivyo nafasi itahesabika kuwa iko wazi na itajazwa kwa kufuata taratibu za uchaguzi wa wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na shule za serikali.Jitahidi kuripoti kabla ya saa 11:00 jioni ili kuondoa usumbufu unaoweza kujitokeza.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

2.1 Sare ya shule

a) Sare ya shule hii ni sketi mbili (2) nyekundu(kitambaa cha suti/estem na. 1) yenye mshono wa **"V"** mbele isiyo na marinda.Mashati mawili(2) ya rangi nyeupe za mikono mirefu.

b) Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na hijabu (umbrella/kijuba) nyeupe 2 zisizo na urembo wala lesi (plain) na nyeusi 2 zisizo na maua. (Jalabibi haziruhusiwi)

c) Sare ya michezo kwa shule hii ni Track suit jozi moja (1) kwa ajili ya michezo na kujihifadhi kwa baridi wakati wa kujisomea usiku. Rangi nyekundu yenye miraba myeupe.Pia Bukta pana kuvuka magoti moja(1) ya michezo ya rangi nyeusi.Vilevile raba jozi moja (1) za michezo.

d) Viatu vya shule ni vya ngozi vyeusi vya kufunga kwa kamba vyenye kisigino kifupi (viatu vya mpira haviruhusiwi)

e) Soksi jozi mbili (2) nyeupe ndefu .

f) Sweta moja (1) rangi ya dark blue yenye "**V"** mbele.

g) Nguo za kushindia (shamba dress) za shule hii ni sketi nyeusi ndefu mbili (2) kitambaa cha suti (esteem).Msono wa solo isiyo na marinda.

h) Tai nyekundu jozi mbili(2)

2.2 ADA NA MICHANGO YA SHULE

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi **70,000/=(**elfu sabini).Unaweza kulipa kiasi cha shilingi **35,000/=(**elfu thelathini na tano) kwa muhula au kulipa ada yote kwa maramoja.Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Namba**: 5021200061,** Jina la Akaunti ni **KONDOA GIRLS' HIGH SCHOOL benki ya NMB.**

NB: Hakikisha unaandika jina la mwanafunzi kwenye pa-in-slip

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

MICHANGO NI KAMA IFUATAVYO:

Na.	MICHANGO	KIASI (TSHS)	MAELEZO
1.	Taaluma	20,000/=	Lipia Benki
2.	Kitambulisho na picha	6,000/=	Lipia Benki
3.	Tahadhari	5,000/=	Lipia Benki
4.	Ukarabati wa samani	15,000/=	Lipia Benki
5.	Huduma ya kwanza na bima ya afya	10,000/=	Lipia benki
6.	Wapishi,walinzi na vibarua wengine	30,000/=	Lipia Benki
7.	Nembo	2,000/=	Lipia benki
8.	Kukodi Godoro kwa muhula	10,000/=	Lipia Benki
9.	Mitihani ya kujipima Mock	20,000/=	Lipia Benki
	JUMLA	**118,000/=**	Lipia benki

Zingatia:

- Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Namba**: 5021100041,** Jina la Akaunti ni **KONDOA GIRLS' HIGH SCHOOL,** benki ya **NMB.**
- Hakikisha unaandika jina la mwanafunzi kwenye pa-in-slip

UTARATIBU WA KULIPA FEDHA YA MAHITAJI YA SHULE (ADA NA MAHITAJI MENGINE.)

Tumia **BENKI ya NMB** kulipa fedha ili kuepuka upotevu. Lipa fedha ya mahitaji ya shule wiki moja kabla ya shule kufunguliwa au kabla ya hapo kama ifuatavyo:-

TUMIA AKAUNTI ZIFUATAZO:

a) KULIPIA KARO/ADA YA SHULE:		**KIASI CHA MALIPO(TSHS) KWA MWAKA/Muhula**
NAMBA YA AKAUNTI	**5021200061**	**Ada 70,000/=kwa mwaka au 35,000/= kwa muhula**
JINA LA AKAUNTI	KONDOA GIRLS' HIGH SCHOOL	
b) KULIPIA MICHANGO MINGINE		**Michango 118,000/=**
NAMBA YA AKAUNTI	**5021100041**	
JINA LA AKAUNTI	KONDOA GIRLS' HIGH SCHOOL	

Zingatia:

- SIKU ya kuripoti hakikisha unaleta **Nakala za Malipo** (Bank Pay-In- Slip) na zikabidhiwe kwa Mhasibu wa shule pindi tu ufikapo shuleni.
- Pamoja na fomu hii, tunakuambatanishia mchoro wa sare ya darasani ambayo ni kitambaa chekundu aina suti na sketi ya kazi ni kitambaa cheusi (aina ya suti) unaweza kushona mwenyewe au kushonea Kondoa kwa mafundi waliopo karibu na shule. Shati, sweta vinapatikana Kondoa Sekondari.
- Tumia Naamba ya wakala **M.PESA 337546 Hezron Enock Lyamba** kwa ajili ya pesa ya matumizi na nauli ya mwanafunzi baada ya kutuma andika jina la mtumaji, aliyetumiwa na kiasi ulichotuma tuma msg. kwenye namba –
- 0753-507580.

c) MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI NI:

i. Mzazi/mlezi anapaswa kumpatia mwanae(mwanafunzi) mahitaji haya yafuatayo:

a) Ream ya karatasi 1(kwa mwaka)

b) Madaftari makubwa (counter books-Quire 3) kumi (10) kwa masomo ya Tahasusi yoyote sayansi au sanaa.(Yanapatikana katika Duka la Shule kwa @Tshs.3000/=)

c) Scientific calculator ya Casio yenye Function 882 au 991 kwa wale wa tahasusi za sayansi tu

d) Oxford Dictionary – Advance learners – 6th Edition kwa wale wa tahasusi za HGL na HKL.

e) Kamusi ya Kiswahili ni kwa ajili ya wale wa machaguo ya HKL na HGK.

f) Kopo la vifaa vya Hisabati (Mathematical Set Instruments) isipokuwa wale wa tahasusi za sanaa(Arts) mfano- HGL,HGK na HKL

g) Kalamu za wino, za risasi, rula na raba.

h) Dissection kit 1 kwa wanafunzi wa Biolojia (zinapatikana kwenye maduka/stationery yanaouza vifaa vya maabara).

i) Ndoo ndogo mbili(2) zenye mifuniko

j) Mashuka mawili(2) ya rangi ya Pinki,blanketi moja(1),foronya moja(1),chandarua kimoja(1).

k) Vyombo vya chakula(sahani,bakuli,kijiko na kikombe).Kamwe, Vyombo vya Plastiki,Kontena haviruhusiwi shuleni.

l) Daftari dogo kwa ajili ya hospital/matibabu

m) Shule haina chakula maalum (special diet).Hivyo mwanafunzi atajigharamikia mwenyewe kama atakuwa na uhitaji huo.

n) Nguo za ndani za kutosha na jozi ya khanga/kitenge

o) Mafuta ya kujipaka,dawa ya meno mswaki,ndala,taulo,toilet paper na dawa ya viatu

p) Viatu vya wazi vya kuvaa baada ya masomo

NB: MZAZI/MLEZI anashauriwa kumnunulia mwanae japo kitabu kimojakimoja kwa masomo atakayosoma hapa shuleni kulingana na tahasusi aliyopangiwa.(orodha imeambatanishwa)

ii. MAHITAJI MENGINE YA KITAALUMA.

Mwanafunzi anayeripoti ahakikishe analeta viambatanisho vya kitaaluma vifuatavyo kwa ajili ya matumizi ya ofisi:

A. Cheti halisi cha kuzaliwa **(Birth certificate)** kiambatane na kivuli/nakala yake.

B. Cheti Halisi cha kuhitimu Kidato cha Nne**(Form Four Leaving Certificate)** pamoja na Kivuli/Nakala yake

C. Hati Halisi ya Matokeo ya Kidato Cha Nne(**Form Four Results Slip**) iambatane na kivuli/Nakala yake .

Zingatia: Taarifa zilizopo kwenye vyeti hivyo zioane na taarifa tulizo nazo juu ya mwanafunzi.

iii. VIFAA VYA USAFI:

Kwa ajili ya kuwafundisha na kuwajengea wanafunzi wetu tabia ya usafi na utunzaji wa mazingira na pia kuweka shule yetu katika hali ya usafi na mazingira ya kuvutia,salama na bora kuishi ,Mwanafunzi afike shuleni siku ya kuripoti na vifaa vya usafi kama inavyojieleza katika jedwali lifuatalo:

NA.	TAHASUSI	AINA YA VIFAA VYA LAZIMA KUVILETA KITAHASUSI			IDADI
1.	**PCM**	1.Ufagio mmoja(1) wa chelewa wenye mpini	2.HARD BLOOM moja(1) (brashi ngumu) yenye mpini	3.Jembe lenye mpini	Vyote Vitatu(3)
2.	**PCB**	1.Ufagio mmoja(1) wa chelewa wenye mpini	SOFT BLOOM moja(1) (brashi nyepesi/ufagio wa ndani) mmoja(1)	3.Jembe lenye mpini	Vyote Vitatu(3)
3.	**CBG**	1.Ufagio mmoja(1) wa chelewa wenye mpini	SOFT BLOOM(brashi nyepesi/ufagio wa ndani) mmoja(1)	3.Jembe lenye mpini	Vyote Vitatu(3)
4.	**HGL**	1.Ufagio mmoja(1) wa chelewa wenye mpini	2.SQUEEZER (ufagio wa kukaushia maji) mmoja(1)	3.Jembe lenye mpini	Vyote Vitatu(3)
5.	**HGK**	1.Ufagio mmoja(1) wa chelewa wenye	2.SQUEEZER (ufagio wa kukaushia maji) mmoja(1)	3.Jembe lenye mpini	Vyote Vitatu(3)

		mpini			
6.	**HKL**	1.Ufagio mmoja(1) wa chelewa wenye mpini	Reki na mpini wake	3.Jembe lenye mpini	Vyote Vitatu(3)

Zingatia: HAKIKISHA UNALETA VIFAA KULINGANA NA MAELEKEZO YA KILA TAHASUSI.Pia kwa wale wa mbali na Kondoa,Vifaa hivyo vinapatikana Kondoa.

iv. **MUHIMU**

Mambo yafuatayo yanasisitizwa tena kwa sababu ya unyeti wake na namna yanavyochangia ama kufikia malengo (yakifuatwa) au kukwamisha kufikia malengo yetu(yakiachwa na kupuuzwa)

a) Ni marufuku mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi, pasi ya umeme au heater hapa shuleni.
b) Ni marufuku mwanafunzi kuja na nguo za nyumbani. Njoo na sare ya shule ulikotoka. Muda wa kuripoti ni Kuanzia saa 1:30 asubuhi. Mwisho wa kuripoti saa 11:00 jioni
c) Hakikisha fomu za viambatisho (A-C) zimejazwa kikamilifu na zirudishwe shuleni.

SHERIA,KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria za shule zimewekwa ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya taifa,shule na ya mwanafunzi mwenyewe.Hivyo,Mzazi/Mlezi na Mwanafunzi ambae ndiye mlengwa haswa anapaswa kuzisoma kwa makini,kuzitafsiri,kuzielewa na kuzitii wakati wote ili malengo yetu yaweze kufanikiwa kwa faida yetu sote.(Sheria hizi zipo kwenye Kiambatanisho Na. …….)

3. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI:

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa siku 90(Tisini) bila taarifa/utoro
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika.Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
ix. Uvutaji wa sigara
x. Uasherati,uhusiano wa jinsi moja,Kuoa au kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xv. Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

KARIBU SANA KONDOA GIRLS' HIGH SCHOOL!!!

……

FLORA NUSSU
MKUU WA SHULE

THE HEADMISTRESS
KONDOA GIRLS HIGH SCHOOL
P.O BOX 193, KONDOA

KIAMBATISHO Nª- A

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI KONDOA

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KONDOA

S. L. P 193, Kondoa-Dodoma Email: kondoagirls@gmail.com **Mob: +255 713 448 417**

FOMU YA KUKUBALI KUSOMA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KONDOA

SEHEMU A:- MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI(Personal Particulars)

(Jaza taarifa kwa umakini,usahihi na ukweli.Hii ni siri yako na Mkuu wa shule Tu)

HABARI ZA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI (kama yalivyo kwenye vyeti vyako)……
2. TAREHE YAKO YA KUZALIWA:……SIKU……MWEZI…… MWAKA……
3. MAHALI ULIPOZALIWA:MKOA……WILAYA…… TARAFA……KATA……KIJIJI/MTAA……
4. DINI…… DHEHEBU:……KABILA:……
5. SHULE NITOKAYO:……NAMBA YA MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA NNE……UFAULU KIDATO CHA NNE: DIVISHENI:……POINTI:……
6. TAHASUSI NILIYOPANGIWA:……UFAULU KWENYE TAHASUSI NI KAMA IFUATAVYO:

MASOMO MATATU(3)				JUMLA YA POINTI
UFAULU				

7. Jina kamili la baba:……kazi ya baba:…… Anwani……Namba ya simu:……AU……
8. Jina kamili la mama:……kazi ya mama:…… Anwani……Namba ya simu:……AU……
9. Unapenda kusomea Fani gani utakapojiunga na Elimu ya Juu?……

SEHEMU B:-HABARI ZINAZOWAHUSU WAZAZI/WALEZI (*Ijwazwe na Mzazi/Mlezi Mwenyewe*)

1. Jina la baba Mzazi/Mlezi……Anwani…… Namba ya simu (*kiganjani*)……kazi ya baba Mzazi/Mlezi…… Mahali anakoishi kwa sasa:Kijiji/Mtaa……wilaya…… Mkoa……
2. Jina la mama mzazi/mlezi:……Anwani:…… Namba ya simu(kiganjani)……kazi ya mama mzazi/mlezi…… Mahali anakoishi kwa sasa:Kijiji/Mtaa……wilaya…… Mkoa……

3. Ndugu/jamaa/marafiki wa karibu na muhimu wanaoweza kuwa msaada kwa mwanafunzi

Wafuatao ni ndugu/rafiki zangu wa karibu ambao wanaweza kunisaidia kama kuna dharura.(Ni vema wakawa watu wazima)

Na.	Jina la ndugu/rafiki	Anwani ya anapopatikana	Simu(INAYOPATIKANA)	Uhusiano
1.				
2.				
3.				

Angalizo: Ni ndugu hao(walioandikwa hapa juu na wazazi/walezi) tu watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi hapa shuleni kwa tarehe na muda utakaopangwa na uongozi wa shule kisha wazazi/walezi kutaarifiwa.

5. Ripoti za maendeleo yake kutoka shuleni ziwe zinatumwa kwa: Ndugu…….
Anwani ya Posta: S.L.P……Simu:…….
Mahusiano yake na Mwanafunzi…….
6. Mwanangu ni mfuasi wa Dini/Dhehebu la……
7. Kituo cha Bus/Trani kilichopo na nyumbani ni……
8. Namba yangu ya simu kwa mawasiliano ya haraka ni……

9.(a)Picha za wazazi/walezi.

Bandika picha(Passport size) ya baba mzazi/mlezi	Bandika picha(Passport size) ya mama mzazi/mlezi
JINA:…….	JINA:…….

9.(b)Picha za ndugu/jamaa/rafiki walioandikwa hapo juu

Bandika picha(Passport size) ya ndugu/jamaa/rafiki	Bandika picha(Passport size) ya ndugu/jamaa/rafiki	Bandika picha(Passport size) ya ndugu/jamaa/rafiki
JINA:…….	JINA:…….	JINA:…….

8. Mimi ……bila kushinikizwa na mtu yoyote,Nikiwa na akili timamu ninakubali kusoma katika shule ya sekondari ya wasichana Kondoa katika Tahasusi ya:…….na ninahidi kusoma na kujifunza kwa bidii ili niweze kufikia malengo yangu,ya shule na ya Taifa.
Pia ninaahidi kutojihusisha kwa aina yoyote kwenye mgomo,fujo au kosa lolote la jinai.
Saini ya mwanafunzi:……tarehe:…….

9. Mimi (Jina la mzazi/mlezi)……nimeridhia mwanagu asome Tahasusi aliiyopangiwa ambayo ni……katika shule ya

sekondari ya Wasichana Kondoa.Vilevile, ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu.Ninakubaliana na sheria za shule na kanuni zake, nitalipa ada na michango ya shule kama ilivyoainishwa na kwa muda mwafaka (mapema) ili kuwezesha shughuli za shule ziweze kufanyika kama zilivyopangwa.

Saini ya Mzazi/Mlezi..... Tarehe.....

.....

FLORA NUSSU
MKUU WA SHULE

THE HEADMISTRESS
KONDOA GIRLS HIGH SCHOOL
P.O BOX 193, KONDOA

Tarehe:.....

KIAMBATISHO Na:-B

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

THE PRESIDENTS' OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

KONDOA TOWN COUNCIL

KONDOA GIRLS' HIGH SCHOOL

P.O.BOX 193, Kondoa-Dodoma Email: kondoagirls@gmail.com **Mob: +255 713 448 417**

The Medical Officer,
……
……
……

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR……
OF FORM V YEAR 2018/2019

Please examine the above mentioned student and complete her form attached below.

Thank you.

THE HEADMISTRESS
KONDOA GIRLS HIGH SCHOOL
P.O BOX 193, KONDOA

……
FLORA NUSSU
HEADMISTRESS

FULL name of student ……

Age……
Blood count (red and white)……
Stool Examination……
Eyes……
Chest……
Spleen……
Abdomen……

Additional information.

Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases……
……

I certify that I have examined the above named student and found her fit/not fit for school admission due to:-

……
……

Name……
Signature……Designation……
Date…… Rubber stamp……

Note: student should bring the Completed form to school/wanafunzi ailete fomu hii shuleni ikwa imejazwa

KIAMBATISHO Nª:- C

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI KONDOA

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KONDOA

S. L. P 193, Kondoa-Dodoma Email: kondoagirls@gmail.com **Mob: +255 713 448 417**

SHERIA ZA SHULE

1. Mwanafunzi anapaswa kuwepo eneo la shule wakati wote isipokuwa anapopata ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu,Makamu Mkuu wa shule au Mkuu wa shule.
2. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare ya shule muda wote wa shule(darasani),wakati wa kutoka nje ya shule,wakati wa kwenda likizo na kurudi.Muda wa kazi za mikono na michezo mwanafunzi atavaa nguo rasmi za kazi/michezo.
3. Mwafunzi anapaswa kutii,kuheshimu na kuthamini kazi za darasani na nje ya darasa nuda wote.Kazi za darasani ni pamoja na kufanja mazoezi ,majaribio ya wiki na/mwezi, mitihani robo muhula,nusu muhula na mitihani ya muhula.
4. Mwanafunzi anatakiwa aitike mwito wa kengelea na mwito mwingine utakaoashiria kumhitaji kwa haraka na kwa nidhamu.
5. Mwanafunzi anaonywa kutumia lugha chafu kama matusi,kejeli,vijembe,mipasho n.k .
6. Kuchelewa kurudi shuleni wakati wa kutoka likizo hata kwa siku moja(1) ni kosa kubwa.Ikitokea mwanafunzi akachelewa aje ameambatana na mzazi/mlezi alieandikishwa shuleni(kwenye kiambatisho –A) na barua iliyopitishwa na **Afisa Elimu Kata** na **Afisa Mtendaji wa mtaa/kijiji/kata** anakotoka,ili kujadili kitendo hicho na ikibidi hatua zaidi za kinidhamu ziweze kuchukuliwa .Ukishindwa kutimiza masharti hayo mwanafunzi atarudishwa nyumbani.Muda wa mwisho kuripoti ni saa 11:00jioni.Wanafunzi wanaotoka mbali ambao lazima watafika usiku waje siku moja kabla watapokelewa.
7. Kutii uongozi na viongozi ni wajibu wa kila mwanafunzi.Mwanafunzi anapaswa kuheshimu uongozi na utawala wa shule,walimu na wafanyakazi wasio-walimu,uongozi wa serikali ya wanafunzi,wanafunzi wenzao na mtu yeyote aliye ndani au/na nje ya shule.
8. Mwanafunzi analazimika kuziheshimu na kuzitii alama za taifa kama vile;-Bendera ya Taifa,Nembo ya Taifa,Wimbo wa Taifa,Fedha ya Nchi,Sikukuu za Taifa n.k
9. Ni marufuku kwa mwanafunzi kujihusisha kwa namna yoyote na siasa shuleni.Haturuhusu mwanafunzi kujihusisha na ushabiki wa kisiasa awapo shuleni.
10. Ni kosa kwa mwanafunzi kugomea adhabu halali inayotekelezwa na mtu mwenye mamlaka juu yake.
11. Nywele fupi zisizozidi urefu wa robo inchi na daima zimechanwa ndizo zitakazoruhusiwa. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kunyoa kipara, panki/kisahani au kuweka dawa ya aina yeyote. Adhabu kali itatolewa kwa yeyote atakayekiuka. Hereni, mkufu, bangili, pete, vipini, kofia, shanga, miwani ya jua, rangi za kucha, hina, lipstick na vitu vingine vitakavyomfanya mwanafunzi kutokuwa na muonekano wa kiuanafunzi haviruhusiwi.

12.Manukato makali (perfumes) hayaruhusiwi kwa mwanafunzi kwani huwasababishia wanafunzi wengine magonjwa ya mapafu kama vile pumu.

13.Mwanafunzi anatakiwa kuonekana Nadhifu na katika Muonekano wa kawaida.Hivyo Mapambo ya aina yoyote kama vile herein,bangili,mikufu, culture(Kalcha)na hirizi hayaruhusiwi.

14.Ni marufuku mwanafunzi kwenda kwenye nyumba za watumishi wa shule kwa sababu yoyote ile kwa muda wowote.

15.Ni kosa kubwa mwanafunzi kuonekana kwenye nyumba za starehe,klabu za usiku, klabu za pombe,pahala popote nchini.Pia kwenye nyumba za wageni kama huna sababu za msingi mathalani uko safarini n.k.Ukigundulika kukiuka hili ,hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako.

16.Wageni wa wanafunzi hawataruhusiwa kuonana na mwanafunzi siku za masomo na/au muda wa masomo.Mgeni yeyote anayetaka kumpa mwanae mahitaji ,atajisajili getini ambapo mlinzi wa zamu atapokea na kukabidhi mzigo huo kwa mwalimu wa zamu.Mwalimu wa zamu atamkabidhi mwafunzi mzigo huo kwa utaratibu maalum utakaokuwa umeandaliwa.Mgeni ahakikishe kuwa;Mzigo wake umesajiliwa kwenye kitabu maalum kwa mlinzi,na atie saini kuepuka usumbufu.Pia amtambue mlinzi .

17.Ni marufuku kwa mzazi/mlezi,ndugu ,jamaa au rafiki kuwasiliana na mwanafunzi kwa kupitia mawasiliano mengine zaidi ya yale yaliyotajwa pale juu.

18.Mwanafunzi haruhusiwi kuolewa,kuwekwa kinyumba,kupata mimba,kujaribu kutoa mimba na/au kutoa mimba,kujihusisha na mahusianao ya jinsia moja na matendo mengine ya aina na mtindo huo.

19.Mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha na unywaji au biashara ya vileo,madawa ya kulevya.

20.Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki au kuwa na simu shuleni.Kosa hili litatafsiri kama hujuma ya kutaka kukwamisha malengo yetu,kuharibu miundo-mbinu ya shule.Mwanafunzi atakaye kamatwa na simu pamoja na hatua nyingine za kinidhamu zitakazochukuliwa, atapewa adhabu kali na kulipia fidia gharama za umeme na uharibifu wa miundombinu ya umeme.

21. Ni marufuku na haramu kwa mwanafunzi yeyote kuandaa,kushawishi au kushiriki kwenye mgomo wowote.Kama kuna tatizo basi litashughulikiwa kwa kufuata utaratibu na ngazi zilizowekwa tangu bweni hadi Baraza la shule.

22.Mgeni atakayeruhusiwa kumwona Mwanafunzi ni yule tu aliyeandikishwa na kubandikwa picha yake kwenye Fomu ya maelekezo ya kujiunga na shule.Kama sio siku Maalumu ya Kutembelewa kwa wanafunzi(Visiting Day) yeyote hatoruhusiwa kumwona mwanafunzi.

23.Ni kosa kwa mwanafunzi kujihusisha na Imani za kishirikina shuleni. Mwanafunzi yeyote atakayejihusisha na Imani za kishirikina(mfano; uchawi) atapata adhabu kali na kuchukuliwa hatua kali za kinidhamu.

24. Mwanafunzi akiharimu Miundombinu ya shule kwa uzembe au makusudi atawajibika kulipia gharama za matengenezo/ukarabati.

25.Ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kutoroka au kuhusika kwa namna yoyote kufanikisha mwanafunzi mwenzake kutoroka shule.

NB: Hizo ni baadhi tu ya sheria za shule.Sheria hizo zinaenda sambamba na kutambua Makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule.

1.AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi……Mzazi/Mlezi wa ……

Ninakiri kuwa nimezisoma sheria za shule nikiwa na mwanangu, tumezijadili kwa pamoja na tumezielewa.Ninakubali kushirikiana na uongozi wa shule katika kila kipengele cha malezi ya mwanangu,na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayoamuliwa na uongozi wa shule pale

mwanangu atakapokiuka mojawapo ya ya sheria na kanuni hizi.Nitalipa ada,michango ya shule, na kuheshimu maelekezo mengine yanaytolewa na shule.

Saini ya mzazi/mlezi .....tarehe:.....

2.AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi .....niliyechaguliwa kujiunga na kidato cha tano(V) katika Tahasusi ya.....katika sekondari ya wasichana Kondoa,nimesoma kwa makini sheria na taratibu za shule nikiwa na wazazi/walezi wangu.Nimejadiliana nao na nimezielewa vema kabisa.Ninahidi kuzitii,kuziheshimu na kuziishi wakati wote bila kusukumwa na nitakuwa tayari kuchukuliwa hatua kali za kinidhamu na uongozi wa shule endapo nitakiuka mojawapo ya sheria na kanuni hizi.

Saini ya mwanafunzi:.....tarehe:.....

3.AHADI NA MAONI YA MKUU WA SHULE

Ninawaahidi ushirikiano wa dhati wazazi/walezi katika malezi ya mtoto wenu.Pi ninamtakia kila la kheri mwanafunzi wangu huyu katiaka safari yake ya kielimu na maisha kwa ujumla

Karibu sana Kondoa Sekondari!!!

.....

FLORA NUSSU

MKUU WA SHULE **Tarehe:.....**

THE HEADMISTRESS
KONDOA GIRLS HIGH SCHOOL
P.O BOX 193, KONDOA

MICHORO YA SARE YA SHULE YA WASICHANA KONDOA
(KITAMBAA CHA SUTI (ESTEM NO.1)



SKETI YA KATI INAYOVUKA MAGOTI.



SKETI NDEFU INAYOISHIA KWENYE KISIGINO.



SKETI NDEFU(SOLO) YENYE UPANA WA KUTOSHA INAYOISHIA KWENYE KISIGINO

ORODHA YA VITABU VYA MASOMO(mzazi unaweza ukamnunulia mwanao)

SOMO LA PHYSICS

1. Nelkon and Parker, Advanced level Physics 7th edition.
2.S. Chand"s principles of physics class XI
3.S. Chand"s principles of physics ,class XII
4.Jim breithaupt, understanding physics 2nd / 4th edition
5.Roger Monastery, Advanced Level physics 4th edition
6.Tom Duncan, Advanced Level physics
7.Calculations , For Advanced level Physics
8. University Physics, New edition

SOMO LA CHEMISTRY

1.physical chemistry, by Delungu (Mzumbe bookshop project 1998)
2. Advanced inorganic chemistry part I and II(Tanzania institute of education).
3.organic Chemistry part 1, The fundamental principles I.L finar (longman LTD)

SOMO LA GEOGRAPHY

1.Principles of physical geography by F J monk house
2. Geography integrated approach by D.waugh
3.Essentials of Practical Geography by Josephat Mwita
4.General geography in diagram by R B burnet
5. Simplified physical Geography(A-LEVEL) by D M
6. Statistical methods and the geographers by s. Gregory

SOMO LA BIOLOGY

1.Biological science;Cambridge university press 1997 3rd edition
2.functional approach by Mbv Robert
3.New Understanding Biology By Suzan Toole
4. Advance biology Principles and application By C J Clegg and Mackean
5.Advanced Biology By Michael kent (2000).Oxford university press uk.

SOMO LA ADVANCED AND BASICAPPLIED MATHEMATICS

1. Basic applied Mathematics by Kiza and Septine I sillem
2. Advanced mathematics by shayo
3.Advanced Mathematics book 1 and 2 by Backhouse
4.Advanced Mathematics Chand's 1 and 2

SOMO LA HISTORY

1.Advanced learners, History form V and six(history 1 and 2)(oxford 2011)
2.Advanced level History for Africa, From Neolithic Revolution to present(zist Kamili 2010)
3. Major events in the world History
4. Advanced level History (Nyambari nyangwine 2007
5.Focus on Modern world history by Japhace, Ponsian, Chakupewa, Mpandije Yusuph P Maunda (2012

SOMO LA GENERAL STUDIES

1.General studies for A- Level certificate form v
2.Contemporary approach for A level general studies notes for form v and six
3.General studies supplementary book for A level and colleges.